

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOZA WA RUVUMA

Simu Nambari. 025-2602256/2602238

Fax No. 2602144

E-mail: [ras.ruvuma@tamisemi.go.tz](mailto:ras.ruvuma@tamisemi.go.tz)

Tovuti: [www.ruvuma.go.tz](http://www.ruvuma.go.tz)



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S. L. P. 74,  
SONGEA

TAARIFA KWA UMMA  
ZIARA YA MHESHIMIWA RAIS – MKOANI RUVUMA

Songea, 03 Aprili, 2019.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma anawatangazia Wananchi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli** atafanya ziara ya kikazi ya siku tano Mkoani Ruvuma kuanzia tarehe 04 – 09/04/2019. Mheshimiwa Rais atawasili na kupokelewa na Viongozi wa Mkoa wa Chama na Serikali Wilayani Tunduru akitokea Mkoa wa Mtwara.

Akiwa Mkoani Ruvuma pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Rais atafanya shughuli zifuatazo:-

Tarehe 04 Aprili, 2019 - Alhamisi:

- Atapokea tāarifa ya maendeleo ya Mkoa na Chama cha Mapinduzi Ikulu Ndogo Tunduru.

Tarehe 05 Aprili, 2019 – Ijumaa:

1. Uzinduzi wa barabara ya Namtumbo – Kilimasera, Matemanga – Tunduru utakaofanyika Tunduru yenye thamani ya **Tshs. Bilioni 148.9**.
2. Uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa Chuo cha VETA Namtumbo wenyе thamani ya **Tshs. 6, 321,320,292/=**.

Tarehe 06 Aprili, 2019 – Jumamosi:

3. Ataweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara za lami za Manispaa ya Songea (km 10.3) zenyе thamani ya **Tshs. 13,164,965,966/=**.
4. Ataweka jiwe la msingi ujenzi wa Kituo cha Mabasi Songea Mjini kinachojengwa Shule ya Tanga katika Manispaa ya Songea chenyе thamani ya **Tshs. 6,189,340,930/=**.

5. Uzinduzi wa mradi wa kusafirisha umeme KV 220 kutoka Makambako hadi Songea wenyе thamani ya **Tshs. 215 Bilioni**.
- Ataongea na wanachi wa Songea katika mukutano wa hadhara utakaofanyika uwanja wa Majimaji Songea.

**Tarehe 07 Aprili, 2019 – Jumapili:**

6. Mheshimiwa Rais atazindua kiwanda cha kuchakata mahindi kilichopo Mlale JKT Wilaya ya Songea chenyе thamani ya **Tshs. 414 Milioni**.
7. Kukagua mradi wa shamba la Gereza Kitai lenye ukubwa wa ekari 650 za mahindi na ekari 100 za maharage.

**Tarehe 08 Aprili, 2019 – Jumatatu:**

8. Ataweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Mbinga – Mbambabay yenyе thamani ya **Tshs. 129,361,352,517/=**.
- Tukio hili litafanyika Mbambabay Wilaya ya Nyasa.
- Kisha ataongea na wananchi wa Wilaya ya Nyasa.

**Tarehe 09 Aprili, 2019 – Jumanne:**

9. Mheshimiwa Rais atazindua Kituo cha Afya Madaba chenyе thamani ya **Tshs. 400,000,000/=**.
- Baada ya hapo ataongea na wananchi wa Madaba. Kisha ataondoka kuelekea Mkoa wa Njombe.

Miradi yote itakayotembelewa na Mheshimiwa Rais ina jumla ya thamani ya **Tshs. 519,750,979,705/=**.

**Mwisho,**

Natoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye maeneo yote ambapo Rais wetu mpendwa atapita kufanya kazi na kuongea na wananchi hadi pale atakapokamilisha ziara yake.

Imetolewa na:

Mhe. Godfrey W. Zambi  
**MKUU WA MKOA LINDI**  
NA  
**KAIMU MKUU WA MKOA WA RUVUMA**